

SHUKRANI

Habari za wakati huu nimekutupia hii kopi kutokna na kwamba umekuwa moja ya mudau unaeniunga mkono katika kununua simulizi zangu , hivyo kwa moyo mkunjufu kabisa naomba nitoe shukrani zangu zote kwa kutambua kipaji changu na hatimae kuniunga mkono .

Ni mimi ISSAI SINGANO(SINGANOJR)

Nakukaribisha kusoma kitabu changu ndani ya mlolongo wa matoleo , tulianza na UMOJA NAMBA TISINI NA SABA(Waraka wa raisi kabla ya kifo) sasa tunaingia kwenye kitabu cha MASAA MAWILI YA KUMBUKUMBU(Kwaninni umoja huu (U-97) umejikita Tanzania .

Theni tunaenda kusoma kitabu cha U-97(BOOK OFF ALL NAMES)

TABLE OF CONTENTS

UTANGULIZI

- SEHEMU YA 01
- SEHEMU YA 02
- SEHEMU YA 03
- SEHEMU YA 04
- SEHEMU YA 05
- SEHEMU YA 06
- SEHEMU YA 07
- SEHEMU YA 08
- SEHEMU YA 09
- SEHEMU YA 10
- SEHEMU YA 11
- SEHEMU YA 12
- SEHEMU YA 13
- SEHEMU YA 14
- SEHEMU YA 15
- SEHEMU YA 16
- SEHEMU YA 17
- SEHEMU YA 18
- SEHEMU YA 19
- SEHEMU YA 20
- SEHEMU YA 21
- SEHEMU YA 22
- SEHEMU YA 23
- SEHEMU YA 24
- SEHEMU YA 25
- SEHEMU YA 26
- SEHEMU YA 27
- SEHEMU YA 28
- SEHEMU YA 29
- SEHEMU YA 30
- SEHEMU YA 31
- SEHEMU YA 32
- SEHEMU YA 34

- SEHEMU YA 35
- SEHEMU YA 36
- SEHEMU YA 37
- SEHEMU YA 39
- SEHEMU YA 40
- SEHEMU YA 41
- SEHEMU YA 42
- SEHEMU YA 43
- SEHEMU YA 44
- SEHEMU YA 45
- SEHEMU YA 46
- SEHEMU YA 47
- SEHEMU YA 48
- SEHEMU YA 49
- SEHEMU YA 50
- SEHEMU YA 51

MASAA MAWILI YA KUMBUKUMBU

2hours of memories.

By

SINGANO JR

Kopi halisi ya kitabu

kimeandikwa mwaka 2020 na kupitiwa upya mwaka 2021.

Haki zote zimehifadhiwa

ONYO

Hauruhusiwi kunakili ama kusambaza kitabu hichi bila idhini ya mwandishi

Jatua kali za kisheria zitachukuliwa.

UTANGULIZI

CIA(Central intelligence Agency) ni idara shirikishi ya kiusalama ndani ya taifa la Marekani , inayofanya kazi kwa kukusanya taarifa zote za kiintelijensia ulimwenguni , taarifa zote hizo baada ya kukusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kina zinapelekwa kwa DNI(Director Of National Intelligence)na huyu DNI anapeleka moja kwa moja kwenda kwa raisi.

Ushawahi kujiuliza tofauti kati ya NSA na CIA basi jibu ni kwamba NSA ni kirefu cha NATIONAL SECURITY AGENCY ni moja ya chombo shirikishi cha kiusalama ndani ya serikali ya Marekani kinachohusika na kukusanya taarifa za kiintelijensia kama ilivyo kwa CIA ila utofauti ni kwamba CIA inahusika na ukusanyaji wa taarifa katika mataifa ya nje(International Intelligence) ambazo ni husianishi , au kwa maneno mengine taarifa ambazo zinahusisha Marekani moja kwa moja au kwa njia isio ya moja kwa moja na hawa CIA wanafanya kazi kwa kusambaza mawakala(Agents) kila kona ya dunia , na hawa ndio wanakusanya taarifa hizo na kisha kuzituma makao makuu ya CIA ambayo yapo Lengley, Virginia na hawa mawakala wanaruhusiwa kushirikiana na vyombo vingine vya kiintelijensia katika kukusanya taarifa zao , kwa mfano MOSSAD, M16 na mashirika mengineyo.

Sasa ukija kwenye NSA ni kwamba misheni au kazi ya hii idara ni kuhakikisha kila intelijensia inayotumwa au inayotoka ndani ya CIA au nje ni ya uhakika , na wanahakikisha taarifa kwa kuvunja vunja kwa kutumia matarakishi yenye teknolojia ya hali ya juu kabisa ambayo yana ulinzi mkubwa.

Yaani ndani ya hiki kitengo mambo yote ya udukuzi wa taarifa na mengineyo husianishi na hayo yanafanyika , kwa hio kila taarifa inayofika hapa mara nyingi inahakikiwa na kutafsiriwa na baada ya hapo ndio inafanyiwa maamuzi .

Kwa hio hawa agent wa NSA sio wadhurulaji kama ilivyo kwa CIA agent, hawa kazi zao wanazifanya wakiwa wamejichimbia katika makao makuu yao yaliopo huko Fort Maede ,Meryland.

CIA hii yenyewe ilianzishwa mwezi wa Tisa mwaka 1947 huku NSA ikiundwa mwezi wa kumi na moja mwaka 1962.

NSA imegawanyika katika makundi mawili kutokana na misheni zao , kundi la kwanza linafahamika kwa jina la SID kirefu chake ni Signal Intelligence Directorate halafu kundi la pili ni IAD yaani Information Assurance Directorate ,

Kundi la kwanza yaani SID kazi yao kubwa ni kutengeneza taarifa zilizokuwa katika mfumo wa mawimbi ya kieletroniki au mfumo ambayo imetumika kama target, yaani kwa mfano mawasiliano , Rada na mifumo yote ya siraha sasa hawa SID ni kuangalia nia na matendo ya taarifa hizo zinahusianaje au zina athari gani kwa Taifa ., yaani kwa mfano wanaweza wakapata taarifa yoyote ile kwa kutumia njia ya kimitandao yaani tuchukulie labda unapanga tukio la kigaidi halafu mawasiliano ya mipango unafanya kupitia mitandao , sasa hawa wajuba kazi yao ni kutafuta hizi taarifa

Sasa baada ya SID kukamilisha kazi yao hawa IAD kazi yao ni kulinda mifumo ya nchi ya kitaarifa .yaani hawa wanazuia wadukuzi kwa kuboresha mifumo yao ya kitaarifa , na unaambiwa mifumo ya ulinzi wa taarifa ya kimarekani ndani ya NSA inakuwa updated kila baada ya sekunde ili kutoruhusu mwanya wowote wa leakage au udukuzi.

CIA yenyewe imegawanyika katika makundi makuu manne kutokana na misheni zao au kazi ndani ya kitengo kuna kundi la kwanza hili linadili na taarifa za site (sehemu husika)duniani kote kundi hili linafahamika kama Directorate of Intelligence, kundi lingine ni National clandestine kazi yake ni kuandaa lakini pia kuongoza misheni zote za siri ,Directorate of support hili nalo kazi yake kubwa ni kutoa sapoti kwa makundi yote matatu na mwisho kuna Directorate of Science and Technology humu sasa ndio kuna maswala ya kiteknolojia katika janja zote .

Sasa hizi idara zinafanyake kazi , jibu ni kwamba kuna wakati hawa NSA wanapata intel(Taarifa) kupitia mitandao sasa baada ya kuipata tuchukulie labda intel hio wameipata katika mawasiliano ya Iraq na Pakistan , Sasa unakuta kuna muda wanataka kuihakiki hii taarifa au ifanyiwe kazi ndio hapo sasa watawahitaji CIA , kwa hio kuna muda hii NSA inashirikiana kwa ukaribu zaidi na FBI pamoja na CIA .

Sasa kama nilivyokuonesha muundo huu wa kiintelijensia wa taifa la Marekani turudi sasa kwenye simulizi yetu .

Lengley, Virginia CIA HQ, 2021 FEBRUARY 0800Am

Ilianza kama siku tulivu ndani ya makao makuu haya , ambayo yalikuwa na pilika pilika za kiusalama, kwani kila mfanyakazi alionekana kuwa bize kuhakikisha kila

mtu anatimiza majukumu yake , kama ilivyokuwa moja ya falsafa kwa wazungu “muda ni mali” basi kwa pilika pilika hizo waliendana na falsafa yao hio .

Basi asubuhi hio ndani ya ofisi ya DCI`s(Director of the Intelligence Agency) alionekana bwana George crispian mkuu wa kitengo cha Directorate of science and Technology akiwa ameambatana na Jane Smith mkuu wa kiitengo cha Directorate of Intelligence , wote asubuhi hio walionekana kuwa na jambo la muhimu la kuripoti kwa mkuu huyo wa CIA bwana Luis Tenet .

Jambo walilokuwa wanazungumzia asubuhi hio ilikuwa ni juu ya misheni iliopewa jina la Dragon X Trail , misheni ambayo ilikuwa ikienda kufanyika nchini Tanzania.

Mbele ya meza hio kubwa iliokuwa imezungukwa na watu wa tatu juu yake kulikuwa na fomu ama bahasha tatu ambapo kila bahasha ilikuwa na taarifa iliokuwa jumuishi juu ya misheni Dragon X ,bahasha namba moja ilikuwa na taarifa kutoka NSA , fomu hii au bahasha ilikuwa imebeba taarifa ya picha , hapa nazungumzia picha kama picha , na picha hizo zilikuwa zikizionyesha ubongo wa binadamu , lakini pia zilikuwa zikionyesha pia Screenshot ya jumbe za meseji kupitia mtandao wa Whatsapp , jumbe hizo zilikuwa zikitoka kwa Profesa au daktari ndani ya hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwenda kwa mkuu (CEO) wa kampuni ya kitehama ifahamikayo kwa jina la EARTH TECH INC , kampuni iliokuwa na makazi yake ndani ya Taifa la Tanzania mkoani Arusha ..

Fomu ya pili ambayo hii sasa haikutoka NSA bali ilikuwa imetoka ndani ya CIA na ilikuwa imewasilishwa kwa DCI na mkuu wa kitengo cha Directorate of intelligence yaani Bi Jane Smith , Fomu hii ilikuwa imejaa nyaraka zenye taarifa kutoka kwa Undercover Agent(wakala) kutoka Tanzania(jina halikutajwa).

Fomu ya tatu hii ilikuwa ipo kwenye meza ya mkuu wa CIA ndani ya fomu hii juu kabisa ya ukurasa wa kwanza kulikuwa na maandishi ya DRAGON X TRAIL MISSION APPROVAL ikiambatana na neno Confidential , fomu hii ilikuwa imetoka kwa Raisi wa USA kupitia ofisi ya DNI kwenda kwa CIA.

Sasa basi ndani ya ofisi watu hao walionekana kujadili jambo , lakini baada ya kama nusu saa hivi , waliongezeka watu wawili watu hawa walikuwa ni wakuu wa vitengo viwili yaanni Directorate of support pamoja na ile ndogo kabisa ya Directorate of clandestine .

Walikuwa wote ni wanaume na baada ya kuungana , walionekana kuwa katika kikao na mwisho wa kikao walionekana walikuwa wakijadili mtu ambae anakwenda kuiongoza misheni hio ya DRAGON X TRAIL.

Lakini kati ya wale watu wawili walioingia ndani ya ofisi hio kwa kuchelewa mmoja alionekana kutoa faili na juu ya hilo faili likuwa na nembo kubwa ya alama ya UMOJA NAMBA TISINI NA SABA yaani U-97 na faili hilo lenyewe likiambatana na neno CONFIDENTIAL

Hii misheni ni nini haswa , kwanini ifanyiwe ndani ya Taifa laTanzania , jibu la jambo hilo linakuja kupitia tukio ambalo ndani ya Taifa lilionekana ni tukio la kawaida kabisa kutokea katika jamiii , lakini kumbe ni jambo ambalo lilikuwa limebeba athari kubwa kwa jamii ..

Tukio hilo linakwenda kwa jina la MASAA MAWILI YA KUMBUKUMBU ni tukio la kisisimua lililotengeneza sababu ya kuundwa kwa misheni iliofahamika kwa jina la DRAGON X TRAIL.

Lakini ni tukio ambalo lilipelekea kufichuka kwa siri kuu ya UMOJA NAMBA TISINI NA SABA siri ya kitabu cha BOOK OF ALL NAMES

Huo ni utangulizi wa kitabu changu kinacho enda kwa jina la MASAA MAWILI YA KUMBUKUMBU

Sasa kwa wewe ambae ushakwisha kusoma UMOJA NAMBA TISINI NA SABA (waraka wa raisi kabla ya kifo) basi nakuomba usome na tukio lililotokea katika kitabu cha MASAA MAWILI YA KUMBUKUMBU ili upate maana halisi ya ya code name U-97 je ni nini maana halisi ya hilo neno , je kuna umoja huo kwenye jamii au duniani kwa ujumla wake basi usisite kusoma.

Mambo makuu mawili utakayo yapata kuyajua katika kitabu hiki ni pamoja na jinsi gani mashirika makubwa ya kimitandao yanavyokagua mawasiliano ya wateja wao wote dunia nzima .

Utapata kujua nini nini kiligunduliwa katika BLUE BOOK project, pia utakuja kugudnua namna projekti hio ilivyo changia uundwaji wa project ya TOP ON FILE project iliokuwa ipo chini ya STAR LABS pamoja na IBM .

Je unataka kujua ni nini kilichonyuma ya DRAGON X TRAIL MISSION hakikisha haukosi kusoma .

NB kitabu hiki kwa sasa kinapatikana kwa njia ya softcopy (PDF,DOC and EPUB) kina season 1&2 kila season ina vipande 50 kila episode inapatikana kwa bei ya ofa 4000 tu mpaka kesho kutwa ambappo itapatikana kwa kila season 6000

Lipia kupitia namba 0687151346 jina ISSAI SINGANO ukishalipia nitumie ujumbe whatsapp au gusa Link hapo chini itakuunganisha moja kwa moja kuwasiliana na mimi.

[Http://wa.me/+255687151346](http://wa.me/+255687151346)